



**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR  
WIZARA YA AFYA  
TAARIFA KWA UMMA**

**MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA NCHINI TAREHE 19 APRIL, 2020**

Wizara ya Afya Zanzibar inatoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa wapya ishirini na tatu (23) wa Corona (COVID – 19) Nchini na kufikia idadi ya wagonjwa hamsini na nane (58) kutoka wagonjwa thelathini na tano (35) ambao tuliowatolea taarifa tarehe 17 Aprili, 2020.

Kati ya wagonjwa wapya, wagonjwa ishirini na moja (21) wanaishi Unguja na wawili (2) wanaishi Pemba. Kati ya hao, wagonjwa ishirini na moja (21) ni Raia wa Tanzania. Wagonjwa wawili (2) ni Raia wa Kigeni, Mmoja (1) ni Raia wa Ufaransa na Mmoja (1) ni Raia wa Cuba na wote wanaishi Zanzibar. Wagonjwa wawili (2) kati ya wagonjwa wapya walifariki nyumbani kabla ya kuchukuliwa vipimo, na kufanya jumla ya wagonjwa waliofariki kwa maambukizi ya Corona kufikia watatu (3).

Serikali kupitia Wizara ya Afya, inaendelea kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu zinazotolewa mara kwa mara, ikiwemo kuosha mikono kwa maji ya kutiririka na sabuni, kuepuka misongamano na kuhairisha safari za nje na ndani ya nchi zisizo za lazima.

Aidha Wizara inaomba Wananchi ambao wana dalili za homa kali. Kukohoa na kupiga chafya kujitokeza katika vituo vyetu vya Afya au kupiga simu namba 190. Ni vyema mgonjwa mwenye dalili za maradhi haya asijichanganye na wagonjwa au watu wengine na tuache tabia ya kujitibu wenyewe kwani kwa kufanya hivyo tutaendelea kueneza maambukizi na vifo vinavyo husiana na ugonjwa huo.

Pia vyombo vya habari vinahimizwa kupata Taarifa za ugonjwa huu wa COVID 19 kutoka Wizara ya Afya.

Ndugu Wananchi, Tuendeleo kumuomba Mwenyezi Mungu azidi kutulinda na atupe nguvu za kupambana na Maradhi haya.

**Hamad Rashid Mohammed (MBM)(MBLW),  
Waziri wa Afya - Zanzibar.**